TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI
SHULE YA SEKONDARI VWAWA
S. L. P 224 MBOZI MBEYA TANZANIA, SIMU 025-2580063 – 0714-101651

KUMB NO. VSS/ B/10 **Tarehe .....**

YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII</u>

Mpendwa mwanafunzi _____
Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO CBG, HGL,HKL na HGK** mwaka **2018/2019** katika shule ya Vwawa. Unatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku **kumi nne (14)** kuanzia tarehe **02/07/2018** kinyume cha hapo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. **Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo**

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha ya vifaa ambavyo lazima uwe navyo, **sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakokuwa mwanafunzi wa shule hii, fomu ya udhibitisho wa uraia wako (unaweza kulete nakala ya cheti cha kuzaliwa), fomu ya udhibitisho wa afya yako, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla hujafika shuleni, pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule**. Kumbuka kipimo cha maendeleo yako ni taaluma, kazi za nje pamoja na nidhamu yako ndani na nje ya shule kwa muda wote utakao kuwa shuleni hapa.

Mzazi/ mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa umakini ili kuepuka usumbufu siku za baadaye. Aidha kwa wanaotoka mbali mahitaji mengi yanapatikana katika duka la shule na soko la Vwawa.

ENEO LA SHULE LIPO: Shule ipo mkoa wa Songwe, wilaya ya Mbozi, Nusu kilomita kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe.

_____
P. W. MAHENGE
MKUU WA SHULE

SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa asijihusishe na makosa yafuatayo hapo chini vinginevyo anaweza kufukuzwa/ kufutwa shule:

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo bila taarifa.
3. Uasherati na Ushoga
4. Ulevi na Matumizi ya madawa ya kulevya
5. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake/walimu/walezi.
6. Uvutaji wa bangi
7. Makosa ya jinai
8. Kupigana na kupiga
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kuolewa au kujihusisha na mapenzi.
12. Kupata mimba, kufanya jaribio la kujiua.
13. Kutoa mimba
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe
17. Kulala nje ya shule bila ruhusa (Utoro)
18. Kuwasha mshumaa bwenini/ kukutwa na kiberiti
19. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa.
20. Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

C: **VIFAA NA MAHITAJI MENGINE**

1. Passport size nne (4) pazia la light blue (blue bahari) nyuma na avae shati la shule/ nyeupe na picha nne tofauti za walezi/wazazi/Ndugu wa karibu.
2. Soksi nyeupe nzito zisiszo na maua jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi na vya kamba jozi mbili visivyo na visingino virefu.
3. Mavazi mengine ni nguo za ndani za kutosha, taulo, blanketi mbili (2), mashuka mawili (2) rangi la light blue (blue bahari), shuka 1 jeupe la kutandika kitanani, (bed cover lisilotariziwa maua yeyote), mto foronya nyeupe na sanduku imara kufuli na chandarua rangi nyeupe.
4. Mwanafunzi aje na sweta rangi ya kijani (Green)(kijani jeshi), kanga mbili. **(Akija na idadi ya nguo zaidi ya hizi atalazimika kuzirudisha nyumbani kwa gharama zake)**
5. Kijiko cha kulia chakula, sahani na kikombe, ndoo ya plastic ya lita ishirini (20) kwa ajili ya kutunza maji ,ndoo ndogo ya lita 10 kwa ajili ya kuogea na galoni (dumu lita 5) kwa ajili ya kutunzia maji yaliyochemshwa ya kunywa.
6. Aje na:

- Chandarua nyeupe kwa ajili ya kujikinga na mbu
- Spring file moja (1) rangi ya kaki.
- Mkebe (mathematical set), calculator kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi
- Madftari makubwa (counter books angalau three (3) quire) za kutosha peni, penseli na rula
- Mwamvuli
- Dissecting kit 1
- Laboratory Coat 1 (white color)
- Begi la kubebea daftari
- Godoro futi 3 kwa sita (6 x 3)
- Shuka bluu bahari pair 2, mto 1.
- Blanketi 1
- Chandarua kimoja
- Toilet papers za kutosha
- "Ream" mbili (2) za karatasi nyeupe (photocopy paper – A_4) mwanafunzi atatakiwa kuleta "ream" moja kwa kila mwaka iletwe muhula wa kwanza wa mwaka)

7. Sare ya shule Sketi mbili za kijani jeshi unaweza ukashona mwenyewe au ukapata hapa shuleni kwa shilingi 30,000/= zote mbili.
8. Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu (Utanunua mwenyewe)
9. Tai 1 inapatikana shuleni Shilingi 2,000/= na T-shirts moja sh. 10,000/=
10. Rangi ya Ijabu ni nyeupe kwa Waislam.
11. Nguo za kazi ni gauni mbili zitapatikana shuleni kwa sh 30,000
12. Track suit rangi nyeusi na raba kwa ajili ya michezo isiyo bana chini.(utanunua mwenyewe)Jembe 1 na Herd bloom {HGL}
13. Jembe moja lenye mpini na mfagio wa chelewa.{HGK na HKL}Jembe 1 na soft Bloom
14. MUHIMU MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA HATI YA MATOKEO (RESULT SLIP) YA KIDATO CHA NNE

ANGALIZO KWA MZAZI/ MLEZI

1. Fedha anazotumiwa mwanafunzi akiwa shuleni zitumwe kwa njia ya posta tu shule itashugulikia kuzichukua. Mwanafunzi hataraushiwa kwenda benki/ posta/ kituo cha mabasi kuchukua fedha zitazotumwa kwa njia hizo.
2. Mtoto akishapokelewa shuleni. Mzazi/Mlezi au ndugu yeyote harusiwi kuja kumwona labda uitwe na uongozi wa shule, kwa maana nyingine " **HAKUNA SIKU YA KUTEMBELEA MWANAFUNZI"**
3. Mwanafunzi harusiwi kuja na simu na kifaa chochote cha simu, vyakula vya aina yoyote na mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mtu wa nje ya shule yafanyike tu kupitia uongozi wa shule.
4. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa **mavazi nadhifu na yenye heshima, asije na suruali, T- shirts zenye maandishi, nguo fupi na inayobana au kuangaza**
5. Barua ya mwanafunzi itakayotiliwa wasiwasi itafunguliwa na uongozi wa shule.

Kiambatanisho

Taarifa binafsi

1. Jina lako kamili lilivyotumika kidato cha nne .....
   Dini/dhehebu .....
2. Jina kamili la Baba Mzazi/Mlezi .....
   Kazi yake .....
   Anwani kamili ya Baba Mzazi/Mlezi.....
   Namba ya simu ya mkononi .....
   Namba yake ya simu ya mezani .....
   Mahali anakoishi Baba Mzazi/ Mlezi: Mkoa.....Wilaya .....
   Tarafa ..... kijiji/mtaa .....

3. Jina kamili la Mama Mzazi/Mlezi .....
   Kazi yake .....
   Anwani kamili ya Mama Mzazi/Mlezi.....
   Namba ya simu ya mkononi .....
   Namba yake ya simu ya mezani .....
   Mahali anakoishi Mama Mzazi/ Mlezi: Mkoa.....Wilaya .....
   Tarafa ..... kijiji/mtaa .....
4. Hapa Songwe nina/ sina ndugu
   Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalona bandika picha zao.
   NB. Adhabu kali itatolewa ukitudanganya.

S.N	Jina lake	Uhusiano	Mahali anakoishi	Anwani na namba yake ya simu	Picha yake
1.					
2.					
3.					
4.					

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mkoa wa .....

Ofisi ya Mkuu wa wilaya,
Wilaya ya .....,
S. L. P .....

Tarehe .....

Mkuu wa shule,
.....
.....
.....

UTHIBITISHO WA URAIA WA MTANZANIA

Nathibitisha kuwa .....(jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa / kwa kuandikishwa

Baba yake (jina kamili) .....
Amezaliwa katika mkoa wa ..... Wilaya ya .....
Tarafa ya ..... kata ya .....
Mama yake (jina kamili) .....
Amezaliwa katika kata ya .....Wilaya ya .....

.....
Mkuu wa Wilaya

NB: kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati kamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni. **Au leta nakala ya cheti cha kuzaliwa baadala ya fomu hii.**

Shule ya sekondari Vwawa

Fomu ya kukubali

1. Sehemu ya mwanafunzi

Mimi .....ninakubali nafasi niliyopewa kidato cha tano mwaka ..... katika shule ya sekondari Vwawa na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea

Anuani yangu ya kudumu ni .....
.....

2. Sehemu ya mzazi / mlezi

Mimi ..... ninakubali mtoto wangu .....
Kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari VWawa na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake wake wa shule na taifa. Na nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma, tabia n amwenendo wa mtoto wangu nikishirikiana na walimu.

Anuani yangu ya kudumu ni .....
.....
Namba ya simu: .....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Sahihi ..... tarehe .....

NB: (fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Vwawa Secondary School,
P.O.BOX 224,
Mbozi
Date: ……..

To:
THE MEDICAL OFFICER,
.....
.....
.....
Please examine **.....**
As to her fitness for pursuing further education at this school.

1. Haemoglobin **.....**
2. P.V.Blooding ……
3. (A) Blooding ……
   (B) Hearing ……
4. Blood Pressure ……
5. Urine for Sugar and Pregnancy tests ……
6. Stool for routine examination ……
7. Asthma ……..
8. Skin diseases ……..
9. Leprosy ……..
10. Pulmonary tuberculosis ……
11. Employs ……
12. Deformity ……..
13. Mental problem ……
14. Comments ……..
    ……..
    ……..
    ……..

.....
DESIGNATION

KANUNI ZA SHULE

A. HESHIMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote wlioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha **fupi zisizopakwa rangi na nyele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi** kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbilia aliko aMkuu anayekuita.
8. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
9. Kuheshimu ukumbi wa mikuitano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika msatri wakati wa kupokea huduma.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na usimame unapouliza au kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote unapokuwa darasani, usitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
14. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zizopo katika jamii.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vya gharama shuleni **kama redio, video, simu za mkononi au kifaa chochote cha simu, hita n.k.**

B. MAHUDHURIO

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyotr vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba na madarasa.

C. MAANDALIO JIONI

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na Jumapili sa 1:30 hadi saa 4:00 usiku. **Mwanafunzi haruhusiwi kukaa au kulala bwenini muda huo ukipatikana adhabu itatolewa dhidi yake.**
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatao kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.

3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya jioni kikamilifu.

D. KUWAHI

Kila mwanafunzi anatkiwa:

1. Kuthamini muda.
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.

E. SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa

1. Maomo darasani
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini.
5. Kwenye maandamano rasmi.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo.
7. Kazi za mikono (**vazi la kazi**)
8. Michezo.

NB: Mwanafunzi harusiwi Kuvaa kofia, mizura, nguo fupi, zenye mipasuo, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa heleni, mikufu bangili, nguo za kubana, viatu vyenye visigino virefu, mapambo mengine yoyote pamoja na sare akiwa shuleni.

F. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:
   (a) Chumba cha walimu (staffroom)
   (b) Ofisi za shule
   (c) Maabara
   (d) Jikoni
   (e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

G. UGONJWA

1. Endapo kutakuwa na tataizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimi wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matroni wa shule, mwalimu mlezi n.k mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitunzwe kwa matroni.
2. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika sehemu maalum kwa kibali cha shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika hospitali ya serikali.

3. Mwanafuzni mwenye matatizo lazima aufahamishe **uongozi wa shule au Matron wa shule,** mara afikapo shuleni.
4. Shule haitoi **CHAKULA MAALUMU (Special diet)** kwa mwanafunzi wagonjwa.

H. ANGALIZO KWA MWANAFUNZI

1. Mwanfunzi harusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano **barua, daftari lenye nyimbo zamapenzi n.k**
3. ni kosa kwa mwanafnzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.

MAHITAJI MUHUMU (ZILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE HAPO CHINI)

A. ADA NA MICHANGO

1. Ada ya shule .....Sh. 70,000/= kwa mwaka au 35,000/= kwa mwaka au 35,000/= kwa muhula {**Akaunti na: 61201000008** }
2. Kuinua taaluma ..... Sh. 20,000/= (Kwa mwaka)
3. Ulinzi/ UPISHI ..... Sh. 30,000/= (Kwa mwaka)
4. Tahadhali ..... Sh. 5,000/=
5. Afya ..... Sh. 10,000/= (Kwa mwaka)
6. Dawati/Ukarabati ..... Sh. 15,000/=
7. Kitambulisho ..... Sh. 6,000/=
8. Nembo ya shule.....Sh. 2,000/=

Akaunti na 61201100007

Jumla Sh. 158,000/=

9. Mzazi atamgharamia mtoto wake nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
11. Viwango tajwa hapo juu vinaweza kubadilika kulingana na gharama za uendeshaji.

Michango hiyo juu ilipwe kupitia akaunti ya **NMB** na mwanafunzi anatakiwa kuja na risiti za malipo ya Benki (**ORIGINAL PAY IN - SLIP**)